Ufafanuzi wa Ridhaa ya Kukubali

Ridhaa ya kukubali ni uamuzi wa kujua, wa hiari, na wa pamoja baina ya washiriki wa kujihusisha na shughuli za kimapenzi. Ridhaa inaweza kutolewa kwa maneno au matendo, bora tu maneno na matendo hayo yatatoa ruhusa wazi kuhusiana na kuwa tayari kujihusisha katika shughuli ya kimapenzi. Kunyamaza au kukosa kukataa, kwenyewe, hakuoneshi kutoa ridhaa. Maana ya ridhaa haibadiliki kulingana na mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa jinsia, au jinsia ya mshiriki.

Ridhaa kwa tendo lolote la kimapenzi au shughuli ya awali ya kimapenzi kati ya au pamoja na mhusika yeyote haimaanishi moja kwa moja ridhaa kutolewa kwa tendo lingine lolote la kimapenzi.

Ridhaa inahitajika bila kujali kana kwamba mtu anayeanzisha tendo hilo ni mlevi wa dawa za kulevya na/au pombe.

Ridhaa huenda ikawa imetolewa hapo awali lakini inaweza kuondolewa wakati wowote.

Ridhaa haiwezi kutolewa mtu akiwa hana uwezo, jambo linalotendeka wakati mtu anakosa uwezo wa kuchagua kushiriki katika shughuli ya kimapenzi akijua. Kukosa uwezo kunaweza kusababishwa na kukosa ufahamu au kuwa usingizini, kufungwa bila hiari, au ikiwa mtu hawezi kutoa ridhaa vinginevyo. Kulingana na kiwango cha kulewa, mtu ambaye ni mlevi wa pombe, dawa za kulevya, au vitu vingine vya kulenya huenda akawa hana uwezo na kwa hivyo hawezi kutoa ridhaa.

Ridhaa haiwezi kutolewa wakati ni tokeo la kulazimishwa, kuogopeshwa, kudhulumiwa, au kutishiwa kudhulumiwa kwa aina yoyote.

Ridhaa inapoondolewa haiwezi kutolewa tena, shughuli ya kimapenzi ni lazima isitishwe.

Msamaha kwa Mashtaka ya Tabia ya Kutumia Dawa za Kulevya na Pombe

Afya na usalama wa kila mwanafunzi katika Rockland Community College ni wa umuhimu mkubwa sana. RCC inatambua kwamba wanafunzi ambao wamekuwa wakinywa pombe na/au kutumia dawa za kulevya (iwe utumizi huo ni wa hiari au sio wa hiari) wakati ambapo dhuluma, ikijumuisha lakini sio tu dhuluma za kinyumbani, dhuluma za uchumba, ufuatiliaji mtu kwa njia isiyo ya kawaida, au shambulizi la kimapenzi, inapotokea huenda wakasita kuripoti matukio hayo kwa ajili ya kuogopa madhara yanayowezekana kwa ajili ya kufanya hivyo. RCC inawahimiza wanafunzi kuripoti sana dhuluma za kinyumbani, dhuluma za uchumba, ufuatiliaji mtu kwa njia isiyo ya kawaida, au shambulizi la kimapenzi kwa maafisa wa asasi. Msamaria mwema au mtu anayeripoti kwa nia nzuri anayefichua tukio lolote la dhuluma za kinyumbani, dhuluma za uchumba, ufuatiliaji mtu kwa njia isiyo ya kawaida, au shambulizi la kimapenzi kwa maafisa wa RCC au mamlaka za utekelezaji sheria hatachukuliwa hatua ya sheria za kinidhani za RCC's kwa ukiukaji sera za utumizi wa pombe na/au dawa za kulevya unaotokea katika au karibu na wakati dhuluma za kinyumbani, dhuluma za uchumba, ufuatiliaji mtu kwa njia isiyo ya kawaida, au shambulizi la kimapenzi lilipotokea.

Haki za Wanafunzi

Wanafunzi wote wana haki ya:

Kutoa ripoti kwa mamlaka za ndani za utekelezaji sheria na/au polisi;

Ufichuzi wa dhuluma za kinyumbani, dhuluma za uchumba, ufuatiliaji mtu kwa njia isiyo ya kawaida, na shambulizi la kimapenzi kushughulikiwa kwa makini;

Kufanya uamuzi kuhusu kana kwamba, au la, watafichua tendo la kijinai au ukiukaji na kushiriki katika mchakato wa kimahakama au kinidhamu na/au mchakato wa haki ya kijinai bila kulazimishwa na asasi;

Kushiriki katika mchakato ambao ni wa haki, usiopendelea upande wowote, na unaotoa ilani tosha na fursa yenye maana ya kusikilizwa;

Kuchukuliwa kwa hadhi na kupokea huduma za afya na huduma za ushauri zenye heshima na za haki kutoka kwa asasi, zinapopatikana;

Kutopendekezewa kwamba mtu anayeripoti amefanya makosa wakati matendo haya ya jinai na ukiukaji yanapotendwa, au angechukua hatua tofauti ili kuepuka matendo hayo ya jinai na ukiukaji;

Kuelezea tukio hilo kwa wawakilishi wachache zaidi iwezekanavyo wa asasi na kutohitajika kurudia rudia maelezo ya tukio hilo bila umuhimu.

Kulindwa dhidi ya kisasi kulipishwa na asasi, mwanafunzi yeyote, mshtakiwa, na/au marafiki wake, familia yake na wanaohusiana ndani ya mamlaka za asasi;

Kukata rufaa katika angalau ngazi moja ya uamuzi;

Kuandamana na mshauri wake anayemchagua ambaye anaweza kumsaidia na kumshauri mtu anayeripoti au mshtakiwa katika mchakato wote wa kimahakama au kinidhamu pamoja na mikutano na kesi zote zinazohusiana na mchakato huo.

Kutumia haki za umaa na kuwa na ndini bila kuingiliwa na mchakato wa kiuchunguzi, haki za kijinai, au kimahakama au kinidhamu wa asasi.

Haki hizi zinatumika bila kujali mbari, rangi, asili ya kitaifa, dini, imani, umri, ulemavu, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, hadhi ya familia, ujauzito, maumbile ya kijenetiki, hadhi ya kijeshi, hadhi ya muathiriwa wa dhuluma za kinyumbani, au hukumu ya kijinai na bila kujali kana kwamba tendo hilo la jinai au ukiukaji linatokea ndani ya bewa, nje ya bewa, au mtu akisomea ughaibuni.

Una haki ya kupiga ripoti kwa Polisi wa Chuo au Maafisa wa Usalama wa Bewa, mamlaka za ndani za utekelezaji sheria, na/au Polisi wa Jimbo au uchague kutopiga ripoti; kuripoti tukio kwa asasi yako; kulindwa na asasi dhidi ya kisasi kulipizwa kwa ajili ya kuripoti tukio; na kupokea usaidizi na rasilimali kutoka kwa asasi yako.